JINA: _____ **NAMBARI** _____

SHULE: _____ **TAREHE:** _____

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

MEI – JUNI 2016

SAA 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA WA KINKIISI AWAMU YA PILI 2016

CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SHULE YA UPILI

Www.Manyamfranchise.Com

MAAGIZO:

a) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*

b) *Swali la kwanza ni la* ***lazima.***

c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani, Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi simulizi.*

d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

e) *Majibu yotw lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

SEHEMU A: - HADITHI FUPI

SWALI LA LAZIMA

1. (a) "... Anaomba tu muda wake wa masomo umalizike, ahitimu arudi kwao. Arudi kwao na kufaidi utajiri wa umaskini wao, ajitenge na umaskini wa utajiri wa Marekani."

i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala. 4)

ii) Huku ukitoa mifano tambua mbinu mbili za lugha katika dondoo hili. (ala. 2)

iii) Fafanua jinsi mwandishi wa hadithi ya Damu Nyeusi anavyodhihirisha kuwa Marekani si peponi kama wanavyofikiria waafrika wengi wanaopania kwenda huko. (ala. 4)

(b) Jadili jinsi ambavyo mwandishi wa hadithi ya Mwana Darubini ameshughulikia maudhui ya dhuluma. (ala. 10)

SEHEMU B: - KIDAGAA KIMEMWOZEA K. WALIBORA

JIBU SWALI LA **2** AU LA **3**.

2. "Atajua lini jinsi dunia inavyozunguka, mtoto huyu?

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (ala. 4)

b) Taja mbinu moja ya lugha inayojitokeza katika kauli hii. (al. 2)

c) Ni maudhui yapi yanayodokezwa na dondoo hili? (ala. 2)

d) Kwa kurejelea maana inayolengwa na msemaji, onyesha jinsi dunia ya Tomoko ilivyozunguka. (ala. 12)

3. Onyesha jinsi mwandishi wa Riwaya ya kidagaa amefanikiwa kutumia mbinu zifuatazo ili kufanikisha kazi yake:

(i) Sadfa (ala. 10)

(ii) Kisengere nyuma (ala. 10)

SEHEMU C:- TAMTHILIA

T. AREGE: MSTAHIKI MEYA

JIBU SWALI LA **4** AU LA **5**.

4. ".... Kwa unyenyekevu tunakuomba kutumia mamlaka hayo."

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (ala. 4)

(b) Taja na kuthibitisha umuhimu mmoja wa msemaji. (ala. 2)

www.Manyamfranchise.com

(c) Mamlaka yanayozungumziwa katika dondoo hili ni yapi. (ala. 2)

(d) Eleza kwa kutoa mifano kutoka kwenye tamthilia jinsi msemewa alivyotumia mamlaka yake vibaya. (ala. 12)

5. Ukosefu wa uwajibikaji ni suala linaloangaziwa na mwandishi wa tamthilia ya Mstahiki Meya. Thibitisha. (ala. 20)

SEHEMU D: USHAIRI

JIBU SWALI LA 6 AU LA 7

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Mwenye nacho wajishasha wajiona kama ndovu.
Kitu kimekulewesha, huutambuwi uwovu.
Wafikiri kisu gutu, hakikati nyama pevu.
Tangu lini muwerevu, akijinyowa mwenyewe?

Tangu ukipate kitu, `megeuka mpumbavu.
Katu huthamini mtu, ambaye kwamba mtovu.
Wafikiri kisu gutu, hakikati nyama pevu?
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Wangapi `meonekana, mibakhili mishupavu.
Waliyo wakijituna, na mwingi usuluhivu.
Leo hawanasi tena, wageukile maivu.
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

kupata kusikughuri, ukajidhani mwerevu
Na hicho chako kiburi, ujuwe ni maangavu
Iko siku itajiri, ujikute mwenye wavu
Tangu lini mwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Kila mwenye kukuonya, uiwate ndiya mbovu
Huchelewi kumminya, kumvunda zake mbavu.
Fanya ambayo wafanya, hutajinyowa mwenyewe.
Ungajidai mwerevu, hutajinyowa mwenyewe.

www.Manyamfranchise.Com

MASWALI

(a) Ni ipi dhamira ya mtunzi wa shairi. (ala. 1)

(b) Pambanua umbo la shairi hili. (ala. 4)

(c) Taja na kufafanua maudhui mawili yanayojitokeza katika ubeti wa kwanza. (ala.2)

(d) Dhihirisha tamathali ya usemi iliyotumiwa katiks mleo wa ubeti wa pilii. (ala. 2)

(e) Eleza idhini ya ushairi. (ala. 4)

(f) Uandike ubeti wa nne katika lugha nathari. (ala.4)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (ala.3)

i) Kitu
ii) Mtovu
iii) Kusikughuri

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Kazi ni kazi
Kazi inazaa mazao
Kazi mbii hakuna
Kazi ni uhai
Kazi hukuza uchumi

Kazi paso uhai
Kazi msingi wa maisha
Kazi kuleta maendeleo

Kazi ni Baraka
Uhai ni Baraka
Uhai ni kazi

Kazi usofanya
Baraka takosa
Na uhai vilevile

Kokoiko! Kuchele!
Kengele ngelengele
Kiumbe wamaka
Kumekucha! Kazi kuhofia
Kusudi blangeti tavuta
Kujigubika gubigubi
Kujisingizia ndwele.

Kazi mzembe hatumani
Ni damuyo kuilaza
Na kuupiga uvivu.

Kazi kutotamani fahamu
Ni kutamani mauti
Na mauti yakikufika
Ole mbwako tajijutia.

Www.Manyamfranchise.Com

MASWALI

a) Kutokana na shairi eleza jinsi kazi na uhai vinavyoenda sambamba. (ala. 3)

b) Toa ujumbe wa shairi hili. (ala.2)

c) Taja na utoe mifano miwili ya tamathali za usemi zilizotumika katika shairi hili. (ala.4)

d) Andika ubeti wa saba kwa lugha nathari. (ala.4)

e) Kwa kutumia mifano, taja sifa tatu za mashairi huru zinazojitokeza katika shairi hili. (ala.3)

f) Toa mfano mmoja wa idhini ya utunzi. (ala.2)

g) Fafanua maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (ala.2)

i. Mbii

ii. Ndwele

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Miviga ni nini? (ala.2)

(b) Eleza sifa nne za miviga. (ala.4)

(c) Mivigha ina umuhimu gani katika jamii? (ala.8)

(d) Ni ipi hasara ya miviga? (ala.4)

(e) Taja mifano miwili ya miviga. (ala.2)

Www.Manyamfranchise.Com